



# MISINGI YA UFUGAJI KUKU WA ASILI









## Mwongozo wa ufugaji bora wa kuku wa asili vijijini

SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE
1984
ARDHI NI HAZINA

Toleo la **PANTIL**

wellcome trust

SNAL

# MISINGI YA UFUGAJI KUKU WA ASILI

## Mwongozo wa ufugaji bora wa kuku wa asili vijijini

Na

AMANDUS P. MUHAIRWA
Idara ya Tiba ya Mifugo na Afya ya Jamii
Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine
Morogoro Tanzania

PETER LAWRENCE MSOFFE
Idara ya Tiba ya Mifugo na Afya ya Jamii
Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine
Morogoro Tanzania

MADUNDO M.A. MTAMBO
Idara ya Tiba ya Mifugo na Afya ya Jamii
Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine
Morogoro Tanzania

GASPAR ASHIMOGO
Idara ya Uchumi Kilimo
Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine
Morogoro Tanzania

© SUA 2008

ISBN No: 978-9987-525-01-0

Mwongozo huu umetolewa na Mradi wa Uboreshaji Maisha kwa Elimu ya Ufugaji wa Kuku wa Asili (ILRP) wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (2008) chini ya ufadhili wa **Wellcome Trust** ya Uingereza.

*Chapisho hili limetolewa kwa ufadhili wa mradi wa PANTIL*

# Utangulizi


Miaka ya karibuni tumeshuhudia ongezeko la nia ya kutumia kuku wa asili kama chombo cha kupunguza na kuondoa umasikini vijijini katika nchi za dunia ya tatu. Hata hivyo taaluma iliyopo hutoa ushauri kwenye mfumo wa uzalishaji mkubwa kibiashara kwa kutumia aina ya kuku wa kisasa kutoka nje ya nchi. Pia mazingira yanayoakisiwa siyo ya mkulima wa kawaida wa kijijini, wa Tanzania.

Mwongozo huu hauhusiki na ufugaji wa kuku wa kisasa kwa sababu tayari kuna elimu ya kutosha ya ufugaji wa kuku wa aina hiyo. Mwongozo huu umeandaliwa kumuwezesha mkulima wa kijijini kusoma na kuelewa kilichomo yeye mwenyewe. Vile vile maafisa ugani na watoaji elimu kwa wakulima vinaweza kutumia mwongozo huu kwa mafunzo ya wafugaji juu ya ufugaji bora wa kuku wa asili. Hata hivyo bado tunashauri mfugaji amuone ofisa ugani kilimo au mifugo wa kijiji kwa ushauri zaidi au ufafanuzi zaidi juu ya yaliyoelezwa humu na ufugaji kuku kijumla.

Kuku wa asili ni nini: Kuku wa asili ni kuku wanaopatikana katika mazingira yetu ya asili; Tunapendelea zaidi kuwaita kuku wa asili kwa sababu ni neno la hadhi zaidi kuliko kuwaita kuku wa kienyeji. Kwani nani kati yetu angependa kuitwa wa kienyeji? Basi ndugu msomaji katika mwongozo huu tuanze kuwapa hadhi inayostahili ndege hawa wenye faida kubwa kwetu.

Mwongozo huu unatumia njia ya hadithi na picha zinazosimuliwa na watu wawili Bi Tetea na Bwana Jogoo. Maswali yanayoulizwa mara kwa mara na wafugaji yametumika kama chachu ya miongozo inayotolewa





# Shukrani

Elimu ni mchanganyiko wa unayofundishwa na unayojifunza. Tunatoa shukurani kwa wote walioshiriki katika kutupatia elimu na tuliojifunza kutoka kwao. Bila kuwasahau wafadhili mbali mbali waliofanikisha utafiti uliotupatia taarifa nyingi zaidi za kuku wa asili hasa katika magonjwa na utunzaji wa kuku hao. Kwa kuwataja baadhi ni **DANIDA**, Mradi wa **TARP II SUA GL-CRSP** na **Wellcome Trust** ya Uingereza inayofadhili mradi wa uboreshaji wa maisha kwa kutumia elimu ya ufugaji wa kuku wa asili, ambao ndiyo umewezesha uchapishaji wa mwongozo huu.

Shukrani za dhati pia zimuendee Bwana Hassan Hussein Ngomango wa Konga Fine Arts, Morogoro kwa kuchora vikaragosi katika andiko hili. Bila kuwasahau madaktari Gaspar Chiwanga, James Mushi na Flora Kajuna kwa maoni yao na kuipitia kazi hii kabla haijachapishwa. Vile vile shukrani nyingi ziwafikie maafisa kilimo wa mradi wa UMADEP kupitia Idara ya Elimu na Ushauri Kilimo SUA, Bwana Innocent Mathias na Bwana Emmanuel Malisa, kwa maoni yao juu ya andiko hili.

Shukrani za ziada ziende kwa mradi wa PANTIL (Programme for Agricultural and Natural Resources Transformation for Improved Livelihoods) kwa kuweza kufanikisha chapisho hili lililowezesha kitabu hiki kuuzwa kwa bei nafuu.

# Yaliyomo


Utangulizi........................................................................................ii

Shukurani........................................................................................iii

1. Faida za Ufugaji Kuku wa Asili..................................................1

2. Mahitaji Muhimu kwa Ufugaji Kuku wa Asili ..........................2

3. Nyumba na Malazi ya Kuku wa Asili..........................................3

4. Chakula na Lishe ya Ziada kwa Kuku wa Asili ..........................8

5. Uzalishaji wa Vifaranga .............................................................13

6. Udhibiti wa Magonjwa ya Kuku..................................................18

7. Mafua Makali ya Ndege ..............................................................24

8. Kuku wa Asili Kama Mradi wa Kuingiza Kipato .......................28

# 1. Faida za Ufugaji Kuku wa Asili



Ninafahamu kuwa unajua faida za kuku wa asili lakini ngoja nikukumbushe kidogo haya yafuatayo;

Kuku wa asili ni chanzo cha haraka cha pesa kwa kuuza kuku au mayai. Kuku wanaweza kabisa kukuongezea kipato na kukuondolea umasikini.

**Nyama ya kuku na mayai ni protini muhimu kwa watoto, familia, wagonjwa hata na wazee.**

Kinyesi chake pia ni mbolea na maganda ya mayai na manyoya ni mapambo.

Lo! Nilitaka kusahau hili kwani katika shughuli za kijadi kuku ni moja ya zawadi au malipo kama mteja hana pesa.





ZAIDI YA HAYO

- Hakuna dini au utamaduni wowote unaozuia kula kuku katika Tanzania. Vile vile kuku wa asili wanapendwa zaidi na walaji mijini na vijijini.
- Ni mradi rahisi kuanza unaoweza kuendeshwa na akina mama, vijana na hata wazee, kwa sababu hauhitaji mtaji mkubwa.
- Je wewe unajua faida zingine zaidi ya hizi? Basi nitajie.


# 2. Mahitaji Muhimu kwa Ufugaji Kuku wa Asili



Unahitaji nini ili uanze kufuga kuku wa asili?
Je, shida yako ni kufuga kuku wa asili kama chanzo cha mapato?

Basi soma, fikiria, uelewe na ujiandae kwa yafuatayo.

**Je una mahali pa kuwaweka kuku?**
Kuku wanahitaji nyumba ya kuishi ili kujikinga na mvua, jua, wanyama pori na wizi.





**Je Unajua wapi utapata huduma na ushauri?**
Kuku hupatwa na magonjwa, mengine huweza kuua kuku wote kwa muda mfupi. Fahamu wapi unaweza kupata msaada wa kitabibu wa mifugo.

**Je utapata wapi kuku wa kufuga?**
Unaweza kupata kuku kwa kununua tetea au vifaranga wakubwa kutoka kwa jirani, rafiki au sokoni.

Palipo na uwezekano nunua kuku waliochanjwa dhidi ya mdonde.




# 3. Nyumba na Malazi ya Kuku wa Asili



Nyumba ni muhimu kumlinda kuku kutokana na wanyama pori, mbwa, paka, wezi , mvua, upepo mkali, na baridi kali wakati wa usiku.

Nyumba pia ni muhimu kwa kuku anayetaga mayai, anayeatamia na anayelea vifaranga.

Somo hili linajadili aina za nyumba zinazowafaa kuku wako.




- Nyumba iwe kwenye kivuli, Paa liwe refu kuruhusu mtu mzima kuingia ndani kufanya usafi.
- Nyumba iwe na uwezo wa kupitisha hewa, hivyo waya au fito ziwekwe kwenye madirisha makubwa kuruhusu hewa kuingia na kuzuia wanyama.
- Mlango uangalie kaskazini kupingana na jua pia uruhusu mtu mzima kuingia ndani.
- Ijengwe kwa gharama nafuu kwa kutumia mbao, mabanzi, matofali ya tope au ya kuchoma.
- Iwe na mlango madhubuti na kufuli kudhibiti vibaka.

## Ndani ya nyumba ya kuku kuwe na nini?

- **Vichanja vya kulala kuku wakati wa usiku**
  - Iwe na umbo la mviringo ili miguu ya kuku itoshe.
- **Viota vya kutagia na kuatamia**
  - Weka kiota kimoja kwa uwiano kwa tetea watano. Ukiwa na tetea kumi weka viota viwili, na kuendelea.
  - Tumia kibuyu, chungu cha zamani au kikapu.
  - Au tumia mbao kwa kipimo cha ujazo wa futi 1.
  - Tumia majivu au dawa ya kuulia wadudu kama 'Akheri powder' kudhibiti wadudu.



*Vichanja vya kuku (bembea) kwa ajili ya kupumzika usiku*



*Viota vya kuatamia vinaweza tengenezwa kwa mabanzi au mbao*


# Aina mbali mbali za nyumba za kuku



Hapa nitaongelea aina za nyumba za kuku na maelezo yake. Chagua nyumba kutokana na mtaji wako, mazingira uliyopo na ubora wake.

Pia nitaeleza juu ya makazi ya kuku wagonjwa na matenga ya kulelea vifaranga.


## Nyumba ya tope



Nyumba ya kuku inaweza kujengwa kwa miti na udongo alimradi iezekwe vizuri kuzuia mvua.

Weka mlango imara wenye kufuli na madirisha yenye nyavu za waya kuzuia wanyama pori, nyoka na paka.

## Nyumba ya matofali ya udongo au kuchoma



Kwa nyumba bora na ya kudumu jenga kwa matofali ya udongo au hata ya kuchoma.

Siliba sakafu na kuta kwa saruji, kisha paka chokaa kuzuia magonjwa na wadudu.

Weka madirisha na milango imara kuzuia wanyama na wezi.

## Nyumba ya kuinuliwa



Nyumba ya kuku inaweza kujengwa kwa mbao na kuninginizwa juu.

Weka sakafu ya wavu au fito zilizo karibu karibu ili kupitisha na kudondosha kinyesi katika nyumba ya jinsi hii.


Iwe na ngazi ili kuwezesha kuku kuingia ndani ya nyumba.

## Kibanda cha kuku wagonjwa na wageni katika banda

Kuku wagonjwa na wageni wawe na nyumba yao maalum. Nyumba ya kutosha kuku wanne au watano kama iliyoonyeshwa hapa ni ya lazima.

Kuku walionunuliwa wawekwe peke yao kwa wiki moja kabla ya kuchanganywa na wengine. Tumia kibanda hiki kwa kuku wagonjwa pia.

Safisha kibanda baada ya kutoa kuku mwagia majivu au paka chokaa, ili kuua vijidudu vinavyosababisha magonjwa.



## Vifaranga kwenye tenga



*Tenga liwekwe ndani wakati wa usiku na kukiwa na mvua au kivulini wakati wa jua usisahau chakula na maji.*

Baada ya kuanguliwa, vifaranga na mama yao wawekwe pamoja katika siku za kwanza.

Baadaye wape vifaranga chakula wakiwa peke yao ndani ya tenga lililofunikwa, watakuwa na uwezo wa kuingia ndani ya tenga na kutoka kirahisi.

Weka gazeti, majani mapana au pumba za mchele sakafuni wakati wa baridi.

Vifaranga walale na mama yao wakati wa usiku.

**Mradi unavyozidi kuendelea tengeneza kibanda cha mbao na waya ambacho husafishika kirahisi na hudumu zaidi.**

Hapo umemaliza kujenga nyumba ya kuku wako.

Jikumbushe mambo ya muhimu katika somo hili.



- **Jenga kwa kutumia vifaa vinavyopatikana katika mazingira yako ili kupunguza gharama.**
- **Nyumba ya mbao ni budi inyanyuliwe juu na kuwekewa wavu au fito kama sakafu yake ili kuruhusu kinyesi kudondoka.**
- **Madirisha yawekewe wavu kuzuia wanyama pori paka na kunguru na wezi.**
- **Weka vichanja ndani ya nyumba na ziwe na muundo rahisi kutolewa nje na kusafisha.**
- **Weka viota kwa ajili ya kutagia.**
- **Vifaranga na mama zao wawekwe nyumba tofauti na kuku wengine wakubwa.**
- **Hakikisha nyumba ya kuku inaingilika na kusafishika kirahisi.**

# Ni wapi upate msaada wa ushauri wa kitaalamu kuhusu ufugaji kuku?



Mifugo pia huugua na hufa. Mfugaji wa kuku ni lazima ujue ni wapi utapata msaada wa kitaalamu kuhusu ufugaji bora, tiba na kinga ya kuku wako.

Mfahamu mtaalamu wa mifugo wa kijiji atakayekuwa akikupa ushauri na huduma ya kinga ya magonjwa na tiba kuku wanapougua.

Wataalamu hawa hupatikana katika ofisi za vijiji, kata au tarafa.

Ni wajibu wako kutoa taarifa juu ya magonjwa na vifo vya kuku wako kwa mtaalamu . Hili ni muhimu kwa faida yako mwenyewe, wafugaji wengine na nchi kwa ujumla.







Huduma za tiba ya mifugo na ushauri pia hutolewa na vituo binafsi vya tiba ya mifugo vilivyopo mijini, ambapo pia dawa na chanjo za mifugo hupatikana.

Hakikisha unakwenda katika duka ambalo lina wataalamu halali wa mifugo.

Jielimishe juu ya ufugaji wa kuku kwa kusoma vitabu, majarida ya ufugaji kuku, na kusikiliza vipindi vya redio vya ukulima na ufugaji.

Tembelea wafugaji wengine waliofanikiwa ili ujifunze toka kwao.



# 4. Chakula na Lishe ya Ziada kwa Kuku wa Asili

## Kwa nini kuku wapewe chakula cha ziada?



Karibu ndugu msomaji katika darasa hili litakalozungumzia juu ya chakula na lishe.

Kuku wa asili wana uwezo mkubwa sana wa kujitafutia chakula. Mimi nitazungumzia utoaji wa chakula cha ziada .

Karibu ujue sababu na maana.

Mahitaji ya lishe ya kuku hubadilika kutokana na umri na kama anataga au hapana.

Vifaranga wanaokuwa huwa na mahitaji makubwa ya protini, ilhali wale wanaotaga huhitaji sana madini ya chokaa.

Vile vile msimu wa kiangazi kuku hukosa vitamini 'A' kwa ajili ya kukosa majani mabichi, na hivyo kuathiri vifaranga.

Virutubisho vya ziada viongezwe kukidhi mahitaji ya kuku.



Wapatie vifaranga nyongeza ya protini kwa kuwapa unga wa dagaa au wadudu kama mchwa kuongeza protini.

Changanya kikombe kimoja cha unga wa dagaa (au vichwa vya dagaa vilivyotwangwa) na vikombe vitano vya pumba na uwape kuku kama ziada.



Kuongeza chokaa wapatie chokaa ya dukani, au maganda ya mayai yaliyotwangwa baada ya kubanikwa kwenye moto, au mifupa ya samaki iliyotwangwa baada ya kubanikwa. Weka katika chombo tofauti na chakula kingine ili kuku wale kadiri wanavyojisikia.



# VYAKULA VYA ZIADA



Lishe ya ziada ni muhimu kwa vifaranga na kuku wanaotaga. Wakati wa upungufu wa chakula kama kiangazi kirefu kuku wote huhitaji lishe ya ziada.

Wape ziada lakini waache kuku wajitafutie na ziada iwe ni ziada.

Kumbuka kuwapa kuku vitamini 'A' ya kununua dukani wakati wa kiangazi kirefu. Vinginevyo hakikisha kuwa wanapata majani ya kijani au mchicha mara kwa mara. Fuata maelezo yafuatayo kutengeneza chakula.

Msingi wa vipimo vilivyoonyeshwa hapa chini ni kuwa kikombe kimoja cha chai (kile kidogo) ni sawa na gramu 200 za uzito kikijazwa hadi juu. Vikombe vitano vya namna hii huweza kutengeneza kilo moja ya uzito.

| Jinsi ya kutengeneza kilo 1 ya chakula | | |
|---|---|---|
|  |  |  |
| Pumba au mahindi ya kuparaza vikombe 4. | Unga wa dagaa kikombe kimoja. | Chaganya sawa sawa hadi dagaa wasionekane kabisa. |
| Vifaranga wadogo hadi umri wa wiki 8. | Weka nusu ya kikombe cha chai kwa siku kwa vifaranga 10 katika wiki ya kwanza ongeza pole pole hadi kufikia v ikombe viwili ifikapo wiki ya nane. | |
| Kuku wanaokua wiki 9 hadi 20. | Vikombe viwili kwa siku kwa kuku 10 ongeza au punguza kutegemeana na uwingi wa kuku. | |
| Kuku wakubwa. | Vikombe viwili na nusu kwa kuku 10 kwa siku. Ongeza au punguza kutegemeana na upatikanaji wa chakula cha kujitafutia. | |

Uchanganyaji niliokuelekeza hapa ni kwa ajili ya kutengeneza kilo moja ya chakula na kwa idadi ya kuku iliyoonyeshwa hapo juu.

Kiasi kilichopendekezwa ni ziada ya kile anachookota nje. Kama kuku wanafungiwa ndani ongeza chakula mara 2 ya kilichopendekezwa hapo juu.

Kama una kuku wengi zaidi, ongeza kilo kwa uwiano ulioonyeshwa hapo juu.

Viazi na mihogo vimenywe na kukatwa katwa vipande vidogo ili kuku waweze kudonoa

**LISHE NJEMA NI AFYA NJEMA - NILISHE NIKULISHE**


# Vyombo vya maji na chakula



Chakula cha ziada kiwekwe katika vyombo ili kupunguza upotevu unaotokana na kumwagika chini.

Tumia mbao au mabanzi kutengeneza vyombo vya kulia.

Pia waweza tumia vyombo vya plastiki vilivyotumika.




Chombo cha maji kinaweza tengenezwa kutokana na makopo ya bati au plastiki.

Chukua ndoo ya plastiki iliyotumika kata na kisu uache urefu wa kidole gumba.

Chukua kopo la zamani la mafuta litoboe tundu na msumari katika upande wa juu.

Jaza maji hadi juu weka mfuniko kisha geuza juu chini.



# Jinsi ya kutengeneza mchwa kwa ajili ya kulisha kuku



Kuku wanapenda sana wadudu hasa mchwa. Je umewahi kujiuliza ni kwa sababu gani? Jibu ni rahisi wanajua kuwa **Wadudu ni chanzo cha protini.** Badala ya kuwaacha wajitafutie wadudu kila siku watengenezee kwa kufuata mtiririko huu. Kwa vifaranga walio kwenye tenga utawasaidia sana kama utawapa mchwa kama ziada ya protini.



Changanya kinyesi cha ngombe na majani makavu, mabua ya mahindi au maranda ya mbao.



Mwagia na maji hadi kila kilichomo kilowane kisha weka katika chombo kama chungu au boksi.



Chukua chombo chako na ukiweke katika njia ya mchwa kama ilivyoonyeshwa hapo juu.



Acha kwa masaa 24 .




Baada ya muda huo mchwa wengi watakuwa wameota ndani ya chombo.



Wape kuku vyote vilivyomo, mwaga katika eneo walipo kuku waanze kula mara moja.

## Kwa lishe bora endelevu zingatia haya



- Tumia vyakula vinavyopatikana katika mazingira yako kuwapa kuku chakula cha ziada.
- Zingatia bei na kiasi kinachohitajika kama ziada ili usipate hasara.
- Punguza idadi ya kuku wakati wa upungufu wa chakula kupunguza hasara.
- Usiweke chakula cha ziada kwa muda mrefu kitaharibika.
- Weka vyakula mbali na ndege pori na panya kuepuka magonjwa.

# 5. Uzalishaji wa Vifaranga



Je, unajua kuwa unaweza kuchagua jogoo na tetea bora kuwa ndiyo wazazi wa kundi lako?


Je wajua kuwa utunzaji bora wa mayai unaweza kukuongezea idadi ya vifaranga?

Somo lifuatalo litajadili juu ya uzalishaji wa vifaranga hasa kwa kulenga kufanya biashara. Vile vile tutaelezea juu ya kuzalisha vifaranga kwa mpigo, ili uweze kuuza kuku kwa mkupuo.

## Sifa za Jogoo Bora

Jogoo bora awe na Umbo kubwa, awe na ukiko mzuri usioangukia upande mmoja, awe mchangamfu.

Zaidi ya hapo awe anapenda kuwa na himaya yake. Utajuaje hilo? Ukimjazia wapinzani atakuwa anapigana badala ya kufuata matetea! Hivyo umweke yeye na matetea 10.



## Tetea Mzuri ni Yupi?



Awe na umbo kubwa, awe na uwezo wa kuatamia, awe na uwezo wa kulea vizuri, na aweze kutaga mayai ya kutosha.

Je unajua kuwa kuna matetea wengine akiona chakula ni mpaka ale ashibe ndiyo anaita watoto wake? Tetea mzuri hujali watoto kwanza.

## Nifanyeje kama sifa za tetea ninazozitaka zimegawanyika kwa tetea zaidi ya mmoja?

Kwa mfano kuku mmoja ni muatamiaji mzuri lakini umbo lake ni dogo, na mwingine ana umbo kubwa (mfano kuku aina ya kuchi) linalofaa kibiashara, lakini siyo mlezi mzuri.

UFUMBUZI:
Mtumie kuku muatamiaji mzuri kuatamia mayai ya kuku mkubwa. Unaweza kuuza mayai ya kuku mwenye umbo dogo, lakini nakushauri kuwa unaweza ukaatamiza mawili au matatu kila muatamio ili uzao wa kuku unaouhitaji isipotee.

## Utunzaji wa Mayai




Umewahi kujiuliza ni kwa sababu gani mayai mengine huwa hayaanguliwi? Sababu ni nyingi lakini mara nyingi tatizo ni;

1. Kumpa tetea mayai mengi kuliko uwezo wake kuatamia.
2. Kumpa kuku mayai yaliyokaa muda mrefu zaidi ya siku 15 baada ya kutagwa.
3. Mayai yalitunzwa sehemu isiyo na hewa ya kutosha.
4. Kuatamiza mayai yaliyovunjika au machafu.

Hakikisha kuku wako wanataga mayai kwenye viota ulivyowawekea katika nyumba yao.

Okota mayai kila siku na kuyahifadhi mahali safi penye hewa ya kutosha. Wakati wa kuatamiza ukifika chagua mayai kuanzia la mwisho mfano 20,19, 18,17, 16, 15,........YAANI LA MWISHO LIWE LA KWANZA.



Kila ukiokota yai lilotagwa siku hiyo liandike namba kwa kalamu ya risasi mfano, 1,2,3,4,5,6 na kuendelea, ndipo ulihifadhi.


Acha yai moja la kumuita kuku aje atagie hapo hapo kesho yake.

Yai lihifadhiwe ili sehemu butu ya yai itazame juu na sehemu iliyochongoka itazame chini.

Mayai yahifadhiwe kwenye kasha ka kuhifadhia la mayai au boksi liliojazwa mchanga mkavu na msafi. Box likatwe kupunguza urefu na mchanga ujazwe hadi juu.

Safisha mayai yaliyochafuka kwa kinyesi kwa kutumia kitambaa chenye spiriti kidogo au kitambaa kikavu. Usisafishe mayai ya kuatamiza kwa maji.

## Vyombo vya kutunzia mayai



Hifadhi mayai katika kasha la dukani au boksi lililkatwa na kujazwa mchanga safi mkavu wa kujengea.

## Vifaranga wakae vipi na kwa muda gani na mama yao?

Mara baada ya kuanguliwa vifaranga ni lazima wakae na mama yao, awatafutie chakula na kuwalinda na maadui wa mchana na usiku. Pia kuwafunika usiku ili wasipate baridi.

Unaweza kuwaweka katika tenga kama lilioonyeshwa hapa na kuwafunika ndani ili wasiende mbali wakati wa mchana. Usisahau chakula na maji ya kunywa.

Hakikisha hawapigwi jua wala kunyeshewa mvua. Wakati wa usiku ni lazima walale pamoja na mama yao.

Watenge na mama yao baada ya miezi miwili ili kumsaidia mama yao aanze tena kutaga. Muweke mama mbali nao ili waweze kuzoea kujitafutia chakula na kuishi peke yao.



*Usisahau kuweka chakula na maji ndani ya tenga kwa ajili ya vifaranga wako.*

# Kuatamiza mayai mengi kwa mpigo



Kuatamiza mayai mengi kwa mpigo ndiyo njia ya kuweza kupata kuku wengi wa kuuza kwa mkupuo. Huu ndiyo msingi wa ujasiriamali katika sekta ya kuku wa asili.

Baada ya kuelewa namna ya kutunza na kuchagua mayai fuata maelekezo haya uweze hata kupata vifaranga 30 kwa mpigo.

1. Kumbuka kuku huweza kuatamia mayai ya kuku mwingine sio lazima mayai yawe ya kwake, pia kuku huatamia mpaka vifaranga vitotolewe.

2. Kwa hiyo kama unataka kuku watano waatamie na kutotoa kwa mpigo fanya yafuatayo
   a. Kuku wa kwanza akianza kuatamia muwekee mayai viza au mayai yasiyo na mbegu mfano mayai ya kuku wa kisasa au kuku asiye na jogoo
   b. Rudia zoezi hilo hadi utakapofikisha kuku watano . Kisha wawekee kuku wote mayai yenye mbegu.
   c. Kama hautakuwa na mayai ya kutosha labda uliyonayo yamekwishakaa zaidi ya wiki unaweza kununua mayai mazuri kutoka kwa mfugaji unayemuamini.
   d. Mpe kila kuku kati ya mayai 10-12.

3. Wakitotoa wote utapata vifaranga kati ya 35-50 ambao baada ya miezi sita au 8 wataweza kuwa tayari kuuzwa.





*Weka viota vya kutosha, viwe visafi na mwagia majivu au dawa ya kuua wadudu, kudhibiti chawa viroboto na utitiri.*

Sasa ndugu msomaji hebu tujikumbushe mambo ya muhimu katika sura hii, ambayo yataweza kuboresha utotoleshaji wa vifaranga na baadaye kuongeza kipato chako.



1. **Kuandaa majike kwa ajili ya uzalishaji.**
2. **Tengeneza sehemu ya faragha kwa ajili ya kutagia mayai (kiota).**
3. **Weka utaratibu wa kuondoa mayai toka kwenye kiota na kuyahifadhi mahali pa wazi, penye hewa ya kutosha.**
4. **Zingatia matunzo bora kwa kuku watagao kwa kuwapa chakula cha ziada na maji ya kutosha (Dagaa, pumba n.k.).**
5. **Wakati wa kuatamia ukifika, chagua mayai yaliyotagwa mwishoni, yasiyo na nyufa, masafi na mwekee kuku idadi ya mayai (8-12) kadri ya mwili wake.**
6. **Zingatia matunzo ya vifaranga, kuvipatia chakula cha ziada, kuviepusha na ajali na wanyama wakali.**
7. **Ongeza idadi ya kuku kadri ya uwezo na nafasi yako. Zingatia idadi ya majogoo isiwe kubwa sana (Jogoo 1 kwa matetea 8-12).**
8. **Chagua watoto wa kuku walio bora kuwa wazazi wa baadae wa zizi lako.**

# 6. Udhibiti wa Magonjwa ya Kuku



Wote tunafahamu kuwa magonjwa ni chanzo kikubwa cha hasara kwa wafugaji.

Somo hili nitazungumzia kinga dhidi ya magonjwa hatari ya kuku wa asili.

Utafiti umeonyesha kuwa udhibiti wa magonjwa haya huzuia vifo vya kuku na kuongeza kipato cha mfugaji.

## MISINGI YA AFYA BORA NA KUZUIA MAGONJWA KWENYE KUKU

Lishe bora huzuia magonjwa wape kuku chakula bora na maji safi.

Ongeza virutubisho vinavyoweza kupungua kama ilivyoelezwa katika somo la lishe.

Safisha vyombo vya chakula na maji kila mara kupunguza vimelea vya magonjwa.



*Osha vyombo vya chakula kwa maji na sabuni kuua vimelea vya magonjwa.*

Usafi: safisha banda la kuku kila mara kuondoa mlundikano wa kinyesi.

Hakikisha kuwa hakuna unyevu ndani ya banda kuua mazalia ya vimelea hatari.

Paka chokaa ya kujengea ukutani kuua vimelea baada ya mlipuko wa magonjwa. Au mara moja kwa mwaka kama hakuna ugonjwa.

Chokaa huua vimelea vya magonjwa, changanya na maji na uipake kama rangi.



*Paka chokaa angalao mara moja kwa mwaka, au baada ya tukio la ugonjwa mkubwa.*

# MAGONJWA HATARI NA DALILI ZAKE, KINGA NA TIBA



Kuku huweza kuathiriwa na magonjwa mengi sana, lakini utafiti umeonyesha kuwa magonjwa ya mdonde, ndui, koksidosisi, upungufu wa vitamini 'A', huongoza katika kuua kuku wa asili vijijini.

Vile vile viroboto, kupe, chawa na utitiri huweza kuua au kuleta usumbufu unaoweza kupunguza utagaji mayai, uatamiaji na ukuaji wa kuku.


Somo hili ninaeleza juu ya magonjwa haya, karibu msomaji uyaelewe haya.

## MDONDO

Huathiri kuku wa umri wowote na huweza kuua kuku wote kijijini. Dalili zake ni;

- Kuku huacha kula, kuharisha na kupumua kwa shida.
- Kutoa kamasi na machozi.
- Kupooza na kuzungusha kichwa na kutembea kinyume nyume.

Ugonjwa husababishwa na virusi hauna dawa ya kutibu LAKINI unaweza kukingwa kabisa kwa chanjo.





## NDUI YA KUKU

Ndui huathiri sana vifaranga wanaokua hasa wakati wa mvua.

- Husababisha vivimbe katika uso, kishungi, shingo kwa kuku vishingo na chini ya mdomo.
- Kuku huwa mchovu na huweza kufa .

Ugonjwa huu husababiswa na virusi na hauna tiba.

Chanjo inapatikana, na ikitumika ipasavyo huzuia kabisa ugonjwa.

## Ukosefu wa Vitamini 'A'

Huathiri zaidi kuku wadogo wanaokua. Dalili zake ni

- Macho huvimba na kutoa uchafu mzito kama sabuni ya kipande iliyolowana.
- Kuku wenye dalili hawaponi na hatimaye hufa.

Mara kwa mara ugonjwa hujitokeza baada ya kipindi kirefu cha kiangazi.

Kinga ni kuwapa kuku mchicha au majani mabichi, mara kwa mara

Wape kuku wote dawa ya vitamini za kuku kutoka dukani kuzuia kujitokeza kwa ugonjwa.

## Koksidiosisi

Huathiri kuku wa umri wowote lakini huua zaidi vifaranga na kuku wanaokuwa.

Kuku hudhoofika, manyoya huvurugika na kuku huwa kama amevaa koti.

Kuku huharisha damu au kinyesi cha kahawia huonekana.

## Minyoo, viroboto, chawa na utitiri

Minyoo hukaa tumboni na ikizidi sana huweza kusababisha kuku kupunguza kutaga, kuharisha na kuku kupoteza uzito.

Viroboto hushambulia kichwa na kunata huku vikinyonya damu. Viroboto huua vifaranga.



Chawa na utitiri hughasi kuku hadi wakashindwa kutaga na kuatamia.
Mwaga majivu katika banda na viota vya kutagia kama kinga kwa kuku wako.

Tumia dawa za kuua wadudu kama '*akheri powder*' au '*sevin dust*' au zinginezo utakazoshauriwa na wataalamu.

Tumia unyoya mmoja wa kuku ulioloweshwa na mafuta ya taa na utumie kupaka katika viroboto kwenye kuku walioshambuliwa.

# CHANJO ZIPI ZITOLEWE KWA KUKU WAKO?

**CHANJO YA MDONDO**

Hii ni lazima kwa kuku wote

Chanjo itolewe mara nne kwa mwaka, yaani itolewe kila baada ya miezi mitatu.

Kwa vifaranga waliozaliwa nje ya wakati wa chanjo wapewe chanjo wakati wowote katika wiki ya tatu halafu waendelee Kuchanjwa na kuku wengine.

Wafugaji wenye kuku wachache wajiunge pamoja na kuchanja pamoja, hii itapunguza gharama kwani chanjo nyingi za madukani zimetengenezwa kwa ajili ya kuku elfu moja.



*Pata chanjo ya mdonde kutoka ofisi za mifugo au maduka rasmi ya dawa za mifugo. Omba ushauri wa jinsi ya kusafirisha na kutunza chanjo za kuku.*



*Chanjo ya ndui isitolewe kwa vifaranga wenye umri wa chini ya mwezi mmoja.*

**CHANJO YA NDUI**

Itolewe tu pale ambapo ndui inaonekana kuwa ni tatizo kwani bei ya chanjo hii ni ghali.

Chanjo itolewe mara moja kwa miezi sita.

Chanjo hii hutolewa kwa njia ya sindano kwenye bawa na inapaswa ifanywe na mtaalamu wa mifugo.

Wafugaji watengeneze ushirika wa kuchanja pamoja ili kupunguza gharama.

**DAWA ZA MINYOO**

Minyoo hutibiwa kwa kuweka dawa za minyoo katika maji ya kunywa.

Tibu minyoo mara moja au mbili kwa mwaka na usafishe mabanda na vyombo kupunguza mashambulizi.

# Utaratibu wa kinga na chanjo za magonjwa katika kuku wa asili




Chanjo hupatikana katika maduka ya dawa za mifugo au kupitia kwa wataalamu wa mifugo wa serikalini.

Ningependa mjue kuwa chanjo na dawa nyingi zinazouzwa zililenga wafugaji wenye kuku wengi. Kwa hiyo kwa wafugaji wenye kuku wachache ninashauri kuunda vikundi vya wafugaji ili kupunguza gharama.

Hebu fikiria chanjo ya kuku elfu moja wakati una kuku 30. kwa nini msijiunge katika kikundi na kuchanga pesa na kuchanja kwa pamoja?

| UGONJWA | KINGA |
|---|---|
| Mdonde | Chanjo ya mdonde kila baada ya miezi mitatu<br>Ukiwa na vifaranga wengi wametotolewa mbali na muda wa chanjo wachanje wakifikisha wiki tatu kisha baadaye waunganishe na utaratibu wako wa kundi lote. |
| Ndui | Chanjo ya sindano itolewe na mtaalamu mara moja kila miezi sita. Mbali na kuku wazazi, kuku wa kuuzwa wanaweza kuchanjwa mara moja tu. Ikiwezekana chanjo hii itolewe kabla ya mvua ndefu kuanza. |
| Upungufu wa vitamini 'A' | Watafutie kuku majani mabichi au hata mchicha mara kwa mara.<br>Kama hakuna majani wape kuku dawa ya vitamin ya kuku kutoka dukani kwa muda wa siku 3 mpaka 5. Dawa za dukani ni za kuku wengi hivyo ni vema zitumike katika makundi. |
| Koksidiosisi | Safisha banda kila siku kuondoa mkusanyiko wa kinyesi. Ukiwa na vifaranga wengi kwa mfano 20 umezalisha kwa mkupuo, Wape kuku dawa za kinga kama *Amprolium* au *sulfa* kwa siku 3 mfululizo mara wafikishapo siku 7 tokea watotolewe. |
| Viroboto/chawa utitiri | Mwaga majivu katika banda na hasa kwenye viota vya kutagia ili kukinga wadudu. Tumia dawa za dukani mfano '*akheri powder*' na '*sevin dust*' kumwagia kuku mwilini na katika mazingira.<br>Paka mafuta ya taa kwenye viroboto vinavyoonekana. |
| Minyoo | Tibu minyoo ya kuku kwa dawa za dukani mara moja au mbili kwa mwaka, ikiwezekana wiki mbili kabla ya kutoa chanjo ya mdonde. |

USIFANYE HAYA



- KULETA KUKU WAPYA BILA KUJUA HISTORIA YA CHANJO WALIPOTOKA.
- KUCHINJA KUKU WAGONJWA.
- KUACHA BANDA CHAFU.
- KUFICHA UGONJWA BILA KUTOA TAARIFA KWA MGHANI WA MIFUGO KIJIJINI.
- KUUZA KUKU WAGONJWA.
- KUNUNUA KUKU WAGONJWA.
- KUTEMBELEA ZIZI LENYE UGONJWA BILA KUCHUKUA TAHADHARI.
- KUTUPA KUKU WALIOKUFA PORINI.
- KUNUNUA CHANJO ZINAZOTEMBEZWA BARABARANI NA WAUZAJI WASIO RASMI.

# 7. Mafua Makali ya Ndege



Je, mbona sijasikia lolote kuhusu ugonjwa huu wa homa ya mafua makali ya ndege au sio muhimu kwa wafugaji wa kuku wa asili?


Marhabaa hapo umenifikisha !
Ugonjwa wa homa ya mafua makali ya ndege ni muhimu kwa ndege jamii zote ikiwa ni pamoja na kuku wa asili. Ni hatari pia kwa afya ya wanadamu, kwani husababisha kifo! Fuatilia yafuatayo ili upate kuelewa juu ya ugonjwa huu:



Ugonjwa huu husababishwa na virusi vya influenza aina ya A vinavyoweza pia kuambukiza wanadamu na nguruwe.

Zipo takribani aina 144 za virusi hivi vya homa ya mafua makali ya ndege, ila kwa sasa ni aina ya H5N1 ndiyo inayosumbua ulimwengu.

Ndege jamii ya bata pori na wa nyumbani, pamoja na ndege waishio kandokando ya bahari, maziwa, na mito huweza kuhifadhi aina zote hizi za virusi wakati mwingine bila wao kuonyesha dalili za ugonjwa.





*Nyama na mayai kutoka kuku walioambukizwa mafua ya ndege ni hatari kwa binadamu.*



*Makamasi na maji maji kutoka kwa kuku mgonjwa husambaza mafua ya ndege.*

**Njia za kusambaa ugonjwa:**
Njia ya hewa (chafya) na njia ya chakula (kula vitu vilivyochafuliwa kwa virusi) na kugusa macho, pua na mdomo kwa vitu vilivyochafuliwa kwa virusi.

**Vyanzo vya maambukizi:**

Kinyesi, damu, mayai, nyama, makamasi na majimaji kutoka kwa kuku mgonjwa huwa vimejaa virusi.

Maambukizi pia hupatikana katika mazingira yaliyochafuliwa kwa virusi.

Maambukizi huweza pia kupatikana kwenye mavazi, vifaa vya kubebea kuku, magari n.k vilivyochafuliwa kwa virusi

**Vikwazo vya maambukizi:**
Usafi wa mabanda na mazingira kwa ujumla.

Kunawa mikono kwa sabuni kila baada ya kugusa kuku wagonjwa au waliokufa.

Kujihadhari wakati wa kuchinja na kutayarisha kuku kwa ajili ya kitoweo.

Kukaa mbali na kuku wagonjwa au waliokufa kwa ugonjwa huu.



*Usafi wa mabanda na mazingira ni njia muhimu ya kukinga mafua ya ndege na magonjwa mengine katika banda lako.*


**Maambukizi kwa watu**
Hadi sasa maambukizi ya homa ya mafua makali ya ndege ni nadra sana, isipokuwa zaidi ya nusu ya watu walioambukizwa wamepoteza maisha. Maambukizi kati ya mtu na mtu bado hayajadhibitishwa.

Kuambukizwa hutokana na kula nyama au mayai yasioyoiva sawasawa.

Pia kugusa kuku wagonjwa au waliokufa kwa ugonjwa huu au wakati wa kuchinja na kutayarisha kuku kwa kitoweo.



*Epuka kuweka vidole machoni baada ya kushika kuku, nyama ya kuku au kinyesi.*



**Mbinu za kukinga kuku:**
Usifuge kuku na mabata katika nyumba moja.

Chanja kuku dhidi ya ugonjwa wa mdondo kurahisisha utambuzi wa ugonjwa.

Kuondoa kuku wote wenye dalili za ugonjwa na waliokufa na kuwazika au kuwachoma moto.

Usafi, kudhibiti nyendo za kuku wasikutane na ndege pori.

Usirudishe nyumbani kuku waliopelekwa sokoni wakakosa soko kwani wanaweza kuleta ugonjwa.

Kuwatenga kuku wageni kwa takribani wiki mbili kabla ya kuwachanganya na kuku wako.

*Bata wasifugwe pamoja na kuku. Bata hubeba virusi hatari vya mdonde na mafua ya ndege bila kupata dalili za magonjwa hayo.*




*Osha mikono kwa maji mengi na sabuni baada ya kushika kuku, nyama yake au kinyesi.*

**Mbinu za kukinga watu:**
Kunawa mikono kwa maji na sabuni.

Kukaa umbali zaidi ya mita moja kutoka kuku wagonjwa au waliokufa kwa ugonjwa.

Kuchinja na kutayarisha kuku wa kitoweo kufuata mbinu za usalama wa afya ikiwa ni pomoja na kuzuia kuguswa na damu, kujishika machoni, mdomoni na puani wakati wa kutayarisha kuku.

Kula kuku aliyepikwa akaiva vizuri.

**Dalili za ugonjwa:**
Ugonjwa huu una dalili sawa kabisa na zile za ugonjwa wa mdondo ndio maana ni muhimu chanjo ifanyike dhidi ya mdondo kama mbinu ya kupambana na homa ya mafua makali ya ndege.

**Wajibu wako katika kuzuia ugonjwa kwa kuku na watu;**

Toa taarifa panapohusika ukiona vifo vya kuku au ndege pori wengi hasa ukiwa umechanja dhidi ya mdondo kwa kuku.

Nenda haraka katika kituo cha afya ukiona dalili za mafua na homa kali mahali ambapo kuku pia wanaumwa au kufa

Usiokote, usinunue wala usile ndege pori waliokufa wenyewe.




*Usiokote mizoga ya ndege waliokufa wenyewe porini, ni hatari kwako pia kwa kuku wako.*

# 8. Kuku wa Asili Kama Mradi wa Kuingiza Kipato



Hebu linganisha wafugaji hawa wawili, mmoja anauza kuku mmoja shilling elfu 8, na wa pili anauza kuku 10 kwa shilingi elfu 5 kila mmoja.

Je, ni nani mjasiriamali kati ya hawa?


Je, ni nani atapata pesa nyingi zaidi?

Kati ya hawa ni yupi anauza kuku kwa ajili ya kupata hela ya kununua sabuni dukani?

Ni yupi anayeweza kuuza kuku na kurudi na kununua saruji kwa ajili ya kusakafia ukuta?

Je wewe uko upande upi?







Kufuga kuku wa asili ni njia mojawapo ya kuweza kujiingizia kipato. Ndugu msomaji vifo kwa wingi na uanguaji mdogo wa mayai ni vikwazo vya uzalishaji.

Kwa kiasi kikubwa msomaji wangu hukuweza kufuga kibiashara kwa sababu hizo, sasa umeweza kudhibiti magonjwa je, una sababu gani ya kutofuga kuku kama chanzo cha kipato?

Je,utauza kuku mmoja mmoja au utauza kuku wengi kwa pamoja kama wapo?
Fuatilia somo hili uweze kujua biashara hii .

# Unaweza kuuza mazao gani kutoka kwenye kuku?



- Kuku hasa vijogoo, ni zao muhimu la kuuza, uza majogoo wasiohitajika pale wanapofikia ukubwa utakaokupa bei nzuri, kuanzia miezi sita. Jogoo mmoja anatosha kuhudumia majike hadi 12, hauhitaji kuwa na majogoo wengi.
- Kuuza kuku kwa makundi ili uweze kupata hela ya kushikika kuliko kuuza kuku mmoja mmoja.
- Kuuza matetea usiyoyahitaji kwa uzalishaji, haya huweza kuuzwa yakifikisha miezi 8.
- Kuuza majike waliozeeka na wasiotaga mayai.
- Mayai yauzwe mapema baada ya kutagwa kama hayahitajiki kwa ajili ya kuatamiza. Kama una matetea ya kutosha uza mayai sokoni mara kwa mara ili uweze kujenga jina wanunuzi wakufahamu.
- Unaweza kuuza mayai ya kuatamiza kwa wanakikundi wenzako, ili kufanikisha uatamizaji wa makundi.
- Boresha zizi lako la kuku uwe na kuku wazuri ili uweze kuuza mayai ya kuatamiza ambayo yanaweza kuwa na bei kubwa zaidi.

Tafuta masoko ya kuku katika mahoteli, sehemu za kuuza vyakula kijijini na mijini na migahawa.

Jitambulishe kuwa unafuga kuku na uelezee idadi unayoweza kuwauzia na kwa muda gani, jitahidi kutoa bei ya ushindani.

## Baada ya kuuza ufanye nini ?



Umeuza kuku 15 kwa bei ya shillingi elfu 4 kila mmoja umepata shillingi elfu sitini. Si fedha nyingi sana lakini si haba!

Je, gharama yako ilikuwa ni kiasi gani? Wewe unajua

Je, uzitumieje fedha hizo ? Najua jibu la swali hilo ni jepesi sana kwani mahitaji ni mengi sana.

Lakini je utaweza kuyamaliza yote wakati huu? Jibu ni hapana. Sasa basi fuata ushauri nitakaoutoa hapa chini.




Shughuli yoyote ya kijasiriamali ni kwa ajili ya kuongeza kipato kwa matumizi ya kila siku.

Tumia fedha kununua vitu unayohitaji kila siku. Fikiria kuboresha nyumba yako, kadiri kipato kinavyoongeza.

Tumia theluthi moja kwa fungu hili, yaani kama mapato ni elfu 60 tumia elfu 20 tu kwa fungu hili.

Kuna usemi kuwa 'NITUNZE NIKUTUNZE' kuku nao wanasema tutunze tukutunze, hivyo tunashauri tumia theluthi nyingine ya pesa kuboresha mradi wako.




Imarisha banda la kuku, nunua dawa na chanjo za kuku, na vifaa vya kutumiwa katika nyumba yao. Hata ikibidi kupata mbegu zingine ama kwa kununua kuku au mayai yenye mbegu bora.

Tunza theluthi nyingine kwa matumizi ya baadaye, kumbuka akiba haiozi.

Kipato kikiongezeka kwa nini usiweke hela benki, fungua akaunti kama hauna.



# Kumbukumbu Je?



MALI BILA DAFTARI HUPOTEA BILA HABARI. Huu ni usemi wa kale na bado ni kweli hadi leo hii.

Somo hili litakupa ushauri juu ya kutunza kumbukumbu za mradi wako, taratibu endelea kufuatilia.

Kufanya mradi wa kuku ni vema ukiwa unaweka kumbukumbu kila siku au angalao mara moja kwa wiki.

Kila siku waangalie kuku wako kuwaona wana hali gani na ni wangapi waliopo, hapo utaelewa kama kuna ugonjwa wa kutibu au tahadhari gani zichukuliwe.


Weka kumbukumbu za matetea, majogoo, umri wakati wa kutaga na kuangua vifaranga.

Weka kumbukumbu za kiasi, bei na siku ya kununua vyakula, kuku au mayai.

Chakula cha ziada unachotumia kiandikwe kwenye kitabu chako cha kumbukumbu.

Andika tarehe ulizochanja kuku dhidi ya mdonde na magonjwa mengineyo.

Andika idadi, tarehe na bei uliyouzia kuku wako.



Mimi ninaweka kumbukumbu za ufugaji wangu katika daftari. Nina kurasa za kumbukumbu za kuku, vyakula na vifaa, na kurasa za chanjo na dawa. Angalia kurasa zifuatazo uone nina vyoviandika.

# Sampuli za karatasi za kumbukumbu

| 1. KUMBUKUMBU ZA KUKU NA UZALISHAJI | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jina la Mfugaji | | Wiki/Tarehe | | | Wiki/Tarehe | | |
| | Kumbukumbu | Idadi | Thamani | Maoni ya ziada | Idadi | Thamani | Maoni ya ziada |
| 1 | Tetea | | | | | | |
| 2 | Jogoo | | | | | | |
| 3 | Vifaranga wadogo | | | | | | |
| 4 | Vifaranga wakubwa (miezi 2-6) | | | | | | |
| 5 | Kuku waliokufa | | | | | | |
| 6 | Mayai yaliyookotwa | | | | | | |
| 7 | Mayai yaliyowekwa kuatamia | | | | | | |
| 8 | Vifaranga vilivyoanguliwa | | | | | | |
| 9 | Jogoo waliouzwa | | | | | | |
| 10 | Tetea waliouzwa | | | | | | |
| 11 | Vifaranga wadogo waliouzwa | | | | | | |
| 12 | Vifaranga wakubwa waliouzwa | | | | | | |
| 13 | Mayai yaliyouzwa | | | | | | |
| 14 | Kuku waliouzwa/au kuliwa | | | | | | |
| 15 | Kuku waliotolewa zawadi | | | | | | |

## 2.KUMBUKUMBU ZA CHANJO NA AFYA MWAKA 200_

| Ugonjwa | Tarehe za chanjo | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Chanjo ya I | Chanjo ya II | Chanjo ya III | Chanjo ya IV |
| MDONDE | | | | |
| Idadi ya waliochanjwa | | | | |
| Idadi ya wasiochanjwa | | | | |
| Maelezo | | | | |
| NDUI | | | | |
| Idadi ya waliochanjwa | | | | |
| Idadi ya wasiochanjwa | | | | |
| Maelezo | | | | |

### Tiba mbali mbali

| | | |
|---|---|---|
| Minyoo | | |
| Vitamini 'A' | | |
| Koksidiosisi | | |
| Mengineyo | | |


## 3. KUMBUKUMBU ZA VIFAA NA VYAKULA

| Kifaa | | Idadi | Thamani/Bei ya kununua | Tarehe Maoni |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Vikapu | | | |
| 2 | Nyumba | | | |
| 3 | Viota | | | |
| 4 | Vyombo vya maji | | | |
| 5 | Vyombo vya chakula | | | |
| 6 | Vifaa vingine | | | |
| Vyakula na Dawa | | | | |
| 1 | Pumba | | | |
| 2 | Dagaa | | | |
| 3 | Unga wa dagaa | | | |
| 4 | Vitamini za kuku | | | |
| 5 | Madini | | | |
| 6 | Dawa za minyoo | | | |
| 7 | Dawa za koksidia | | | |

Njia rahisi ni kununua daftari n kunakili jedwali hilo hapo juu. Tengeneza nakala za kutosha kuandika hata mwezi mmoja upunguze kazi ya kunakili kila siku. Mwombe mtoto akusaidie kuchora atafurahia na kujifunza pia. Fanya hivyo pia kwa sampuli zifuatazo.

# Mambo ya kukumbuka ili uandae mpango wa uzalishaji kibiashara





Jogoo mmoja anatosha kwa tetea 8 hadi 12 unaweza kupanga uzalishaji na uuzaji wako kwa idadi hiyo.

Tetea ana uwezo wa kutaga mayai mpaka 30 akilishwa vizuri na kama mayai yatakuwa yakiondolewa kwenye kiota.

Kwa uatamiaji na utotoleshaji mzuri, mpe tetea mayai 10 mpaka 12.

Matunzo mazuri kinga za magonjwa na ajali zitakuhakikishia kuwa vifaranga angalao 8 kati ya 10 walioanguliwa wanakuwa hadi kufikia uzito wa kuuzwa.

Ukiwa na tetea watano unaweza kuuza hadi kuku 30 kwa mwaka. Hivyo tetea 10 watakuwezesha kuuza hadi kuku 60 kwa mwaka.

## Zingatia haya ili upate faida zaidi

- Lenga soko sikukuu za mwisho wa mwaka na zinginezo ambapo kuku huuzwa zaidi.
- Jiunge au shirikiana na wenzako kuunda kikundi cha wafuga kuku ili muweze:
    1. Kuchanja pamoja kupunguza gharama.
    2. Kutafuta masoko pamoja
    3. Kupasiana wateja kama hauna kuku wakati huo
    4. Kuweza kujitambulisha kwa masoko kwamba kijiji chenu kina kuku wa kuuzwa kibiashara.
    5. Kuwa na sauti moja katika kupanga bei.
- Tafuta masoko ili ujenge jina kwa wanunuzi wakubwa.

ISBN No: 978-9987-525-01-0

TOLEO LA UFADHILI WA MRADI WA PANTIL WA CHUO KIKUU CHA KILIMO CHA SOKOINE.

Imechapwa na: Bimana Stationers & General Supplies Ltd.
S.L.P 6639, Dar es Salaam, Tanzania.